KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
DAYOSISI YA KASKAZINI MASHARIKI
SHULE YA SEKONDARI LWANDAI
S.L.P. 01, MLALO, SIMU. 0784 - 333680, 0688-0247725, 0659-891855
E – Mail lwandai@ned-elct.org

**02/ 06/ 2021**

# MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)

Mzazi/mlezi wa:
……………………………….
……………………………….

*Salaamu katika pendo lake Bwana wetu Yesu Kristo!*

## 1.0 KUJIUNGA NA KIDATO CHA SITA (VI) MWAKA 2021. (mchepuo ………………. )

Napenda kuchukua fursa hii kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha Sita 2021/2022 katika Shule ya Sekondari Lwandai. Nakupongeza sana kwa kupata nafasi hii. Karibu Lwandai!

Shule hii ni miongoni mwa Shule zinazomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Dayosisi ya Kaskazini Mashariki. Pamoja na kutoa Elimu kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, taratibu na Kanuni za shule zinatoa umuhimu wa kipekee kwenye jambo hili na kwenye maendeleo ya kitaaluma.

## 2.0 MAISHA YA SHULE.

2.1 Shule ya Sekondari Lwandai ni ya mchanganyiko wa wavulana na wasichana (Co – Education). Ni wazi kwamba maisha ya Shule pamoja na sheria yanazingatia mchanganyiko huo. Mwanafunzi atatakiwa kufuata sheria, taratibu na Kanuni za Shule, vinginevyo hatavumiliwa.

2.2 Inatazamiwa kwamba mwanafunzi aliyejiunga na Shule hii atakuwa ni mwenye nidhamu ya hali ya juu. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika hali ya kiuwanafunzi, yaani apunguze nywele kwa heshima (asinyoe kipara) kukata kucha, na kunyoa ndevu vizuri(wavulana) Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na nguo za aina yoyote zaidi ya zile zilizoagizwa, pia huruhusiwi kuleta vyombo vya muziki vya aina yoyote. **Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu**. Mwanafunzi akibainika kuwa na vitu vilivyotajwa hapo juu atafukuzwa shule.

2.3 Mwanafunzi atakayekubali kujiunga na shule hii atatakiwa kutii na kukubali sheria, taratibu na kanuni za Shule. Mara mwanafunzi afikapo Shuleni, mzazi na mwanafunzi watajaza mkataba, kuonyesha na kukiri kwamba atatii na kukubali na kufuata sheria, taratibu na kanuni zote za Shule zilizopo, na kwa kadiri zitakavyo kuwa zikirekebishwa, kufuatana na mahitaji ya wakati.

## 3.0 TAREHE YA KUFUNGUA SHULE.

Shule itafunguliwa tarehe **03 /07/2021** siku ya Jumamosi kuanzia saa 8 mchana wanafunzi wataanza kupokelewa. Ni muhimu sana kufika siku iliyopangwa kwani masomo yataanza mara moja, na mwanafunzi atakayechelewa nafasi yake itatolewa kwa mwanafunzi mwingine.

### 3.1 JINSI YA KUFIKA SHULE (USAFIRI)

- Kwa wale wanaotoka Dar es Salaam, wanaweza kusafiri na Mabasi ya**Shambalai Bus Service Kibomboi na Maning Nice.**

  Mabasi haya yote yanapatikana stendi ya Mabasi Ubungo Dar es Salaam, yanaanza safari saa kumi na mbili asubuhi.
- Wale wa Mikoa ya **Kilimanjaro, Arusha na Manyara**, wapande mabasi ya **Chakito na Kibomboi** yanayotoka Arusha mpaka Mlalo – Lwandai.
- Wale wa **Tanga** wanashauriwa kupanda mabasi ya **Ngwelo**, **Mtembezi na Mwaju.**

Kila mwanafunzi atatakiwa kufika na mzazi/mlezi (Baba /mama) mwenye uthibitisho. Hakuna mwanafunzi awaye yeyote atakayepokelewa akiwa peke yake.

## 4.0 ADA PAMOJA NA GHARAMA ZA MITIHANI KIDATO CHA SITA (VI) 2021/2022 NI TSHS. 1,843,000/= KWA MWAKA.

Ada italipwa kwa awamu nne kama ifuatavyo. (Jedwali na. 1)

| KIDATO | AWAMU YA I | AWAMU YA II | AWAMU YA III | AWAMU YA IV | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| VI | 843,000/= | 350,000/= | 450,000/= | 200,000/= | 1,843,000/= |
| TAREHE | JULAI,2021 | SEPTE, 2021 | JANUARI, 2022 | MACHI, 2022 | |

Pesa ikishalipwa benki haitarudishwa (Non –refundable )

### 4.1 SARE ZA SHULE

**A. SARE ZA DARASANI**

**I)WAVULANA:**

(a). Kila mwanafunzi anapaswa kuja na sare za shule. Suruali nyeusi mbili (2) na mashati meupe ya mikono mirefu mawili.

(b). Aje na Viatu vya ngozi visivyo na urembo, viwe vyeusi vya kufunga na kamba, visivyo na visigino virefu na soksi nyeupe au za rangi moja yoyote.

(c).Atapatiwa Sweta, Tai, T-Shirt, na kitambulisho hapa shuleni.

**II) WASICHANA:**

(a) Kila mwanafunzi anapaswa kuja na sare za shule, sketi mbili za rangi ya khaki nzito na mashati meupe mawili mikono mirefu.

(b) Aje na Viatu vya ngozi visivyo na urembo wala visigino na viwe vyeusi vya kufunga na kamba na soksi nyeupe.

(c) Atapatiwa Sweta, Tai, T-Shirt na kitambulisho hapa shuleni.

### MAHITAJI MENGINE

**A) VIFAA BINAFSI KWA KILA MWANAFUNZI.**

(a) Aje na vifa vya usafi (Soft broom, Jembe, Fagio la chelewa lenye mpini na ndoo.

(b) Suruali mbili za kuvaa nje ya darasa rangi ya rangi ya kijivu( **Light Grey)** ( Kwa wavulana tu) au magauni 2 rangi ya kijivu (**Light grey)** mshono wa debe na marinda yanayoanzia kiunoni kwa wasichana. ) ( **AVAE WAKATI WA KURIPOTI SHULE**).

(c) Shuka mbili za rangi ya **Light Blue** pamoja na Blanket moja.

(d) Godoro, Mto pamoja na Foronya mbili rangi ya **Light blue**
(e) Nguo za michezo, T. Shirt mbili na bukta mbili.
(f) Sketi za kuzungusha kwenye bukta (wasichana)
(g) Raba rangi nyeupe au nyeusi.
(h) Aje na Spring file nne (4) kwa ajili ya kutunzia mitihani yake pamoja na passport size 4.
(i) **Aje na madaftari nane (8) za masomo yake (Counter Books quire 3 au 4**)
(j) Aje na Sweta au Jaketi kwa ajili ya baridi lisiwe na maandishi au picha, nguo hizi zinavaliwa nje ya darasa.
(k) Kila mwanafunzi aje na **OXFORD DICTIONERY** kwa wale wa Mchepuo wa Lugha na Wale wa Mchepuo wa Sayansi waje na **SCIENTIFIC OXFORD DICTIONERY** na **Scientific Non programmable Calculator (f(x)82 – f(x)991 kama muongozo wa Necta unavyotaka)**
(l) Aje na vitabu vya michepuo kama ifuatavyo:-

- **Mchepuo wa Sayansi (Science).**
  (1) Biological Science (D.J. Taylor, N. P. O. Green, G. W. Stout)
  (2) Chemistry (S. Chand's volume I & II)
  (3) Principle of Physics (S. Chand's volume I & II)
  (4) Pure Maths (S. Chand's volume I, II & III)

- **Mchepuo wa Sayansi ya Jamii (Arts).**
  (1) English Language (Contemporary English for A-Level Form V & VI second edition by Francis Mnyawi), A-Level Literature(an essential guide by Nicholous Asheli)
  (2) History (Essential in advanced history paper I & II by Salehe Yasini)
  (3) Economics I & II (Essential for A-Level Economics by Ambrose odhiambo)
  (4) Kiswahili: Nadharia na Tahakiki ya fasihi kidato cha V & VI, Nadharia ya fasihi (kiswahili 2) Kidato cha V & VI fasihi kwa ujumla.
  (5) Geography: (I) Physical Geography by D. T. Msabila.
  (II) Human and economic Geography by D. T. Msabila.
  (III) Practical Geography by Zisti Kamili.

(m) Aje na vyombo vya chakula (kikombe, sahani, bakuli na kijiko).
(n) Aje na fedha za matumizi na nauli ambazo atakabidhi zote kwenye ofisi ya mhasibu, fedha hizo atapewa mara moja kwa wiki au wakati wa dharura.
(o) Aje na mwamvuli mdogo wa kukunja na tochi/ taa ndogo ya Solar au betri.
(p) Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na **REAM 2 saizi ya A4. Muhula** wa kwanza **Ream 1** na Muhula wa pili **Ream 1.**
**(q)** Aje na vitabu vya masomo yake ya **TAHASUSI (COMBINATION)**
(r) Aje na kitabu cha nyimbo (Tumwabudu Mungu Wetu) au fedha Tsh. 15,000/= (aje nayo mkono).
(s) Aje na Bima ya afya au Tsh. 10,000/= kwa ajili ya bima ya afya (aje nayo mkomoni)

**NB**: Mavazi ambayo mwanafunzi anapaswa kuwa nayo ni:

- **Wasichana:** Waje na magauni mawili ya rangi ya Kijivu mpauko (Light Grey) mshono wa debe, marinda ya pasi yaanzie kiunoni na underskirt, mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine zaidi ya hizi zilizoagizwa. (Kitambaa kizito **(AVAE WAKATI WA KURIPOTI SHULE** )
- **Wavulana:** Waje na suruali mbili au zaidi rangi ya Kijivu mpauko (Light Grey ) na T. Shirt mbili rangi nyeusi, zisizo na maandishi yoyote. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine zaidi ya hizi zilizoagizwa.
  (**AVAE WAKATI WA KURIPOTI SHULE** )

- Mahitaji hayo yote hapo juu ni lazima kila mmoja awe nayo na ukaguzi utafanyika mara mwanafunzi afikapo shuleni.

## NAMNA YA KULIPIA

Fedha taslimu haipokelewi, tafadhali ingiza fedha yako Bank halafu njoo na Pay – In – Slip. Mwanafunzi hatapokelewa asipoleta Pay- In –Slip, **HALISI.**

**Awamu ya kwanza ada ilipwe TSH 843,000/=. Ada ilipwe kwenye akaunti ifuatayo.**
**NMB LUSHOTO**
**NED – ELCT LWANDAI SECONDARY SCHOOL**
**A/C No. 41603300003.**

5.0 HITIMISHO:

Pamoja na barua hii ya maagizo ya kujiunga tunaambatanisha fomu ya kuthibitisha nafasi yako ya kujiunga na Shule ya Sekondari Lwandai. Tafadhali jaza mapema na utume kwa Mkuu wa Shule haraka.

*"KUMCHA BWANA NI CHANZO CHA MAARIFA". (Mithali 1: 7a)*

SHULE YA SEKONDARI LWANDAI • DAYOSISI YA KASKAZINI MASHARIKI-K.K.K.T. • S.L.P. 1 MLALO TANZANIA.

……………………
MCH. DANIEL A. MWARABU
MKUU WA SHULE.

A1

## SEHEMU YA SHERIA ZA SHULE.

Lengo la shule ni kutoa vijana walioelimika vizuri na wenye TABIA NJEMA INAYOZINGATIA MAADILI MEMA. Wanatakiwa kuonyesha jinsi gani wanaweza kutumia UJUZI na MAARIFA waliyoyapata kwa manufaa ya Taifa na manufaa yao binafsi.

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria Sala ya asubuhi na jioni bila kukosa.

2. Unatakiwa kuzingatia ratiba ya Shule/masomo na taratibu zote za shule kama zitakavyotolewa kwenye baraza la shule wakati wa "Orientation week"

3. Ni marufuku kutumia madawa ya kulevya, vileo vya aina yoyote, sigara au bangi. Yeyote atakayedhaniwa au kukamatwa atafukuzwa shule mara moja.

4. Ni marufuku kwa mwanafunzi kushiriki kwa vitendo au mawazo yafuatayo ambayo yanaweza kumfukuzisha shule:
   i) Migomo ya aina yoyote
   ii) Utoaji mimba , kushawishi kuharibu mimba au kumpa mimba mwanafunzi.
   iii) Ngono, Utoro wa aina yoyote
   iv) Maandamano yasiyo halali na lugha chafu za matusi
   v) Wizi wa aina yeyote
   vi) Kupigana na wanafunzi/Mwalimu au mfanyakazi wa shule, kutoa lugha chafu, wizi na uharibifu wa mali za binafsi na za shule.
   Mwanafunzi ukibainika kuvunja hayo hapo juu utafukuzwa shule.

5. **Kila mwanafunzi anatakiwa kufikia kiwango cha alama za kufaulu katika masomo, kiwango hicho ni Marks 55 kwa mhula. Hii inamaanisha mazoezi ya kila siku, majaribio na mtihani wa muhula. Mwanafunzi asipofikia wastani atalazimika kurudia kidato au kuhama shule.**

6. Mwanafunzi atatakiwa kulipa Ada na Michango ya Shule mara tu afikapo Shule. Yeyote atakayebaki na ada mfukoni atarudishwa nyumbani mara moja.

7. Ni marufuku kabisa kufuga ndevu au nywele ndefu. Mitindo ya nywele itakuwa ni ile iliyokubaliwa na Shule. Usukaji, nywele hauruhusiwi kabisa.

8. Uongozi wa Shule unayo mamlaka ya kufungua barua ya mwanafunzi na kuikagua mizigo iwapo kuna haja ya kufanya hivyo.

9. Mawasiliano yoyote ama taarifa zozote kati ya mwanafunzi na jamaa yake lazima yafanyike kupitia uongozi wa Shule.

10. Mwanafunzi haruhusiwi kukaribisha au kupokea mgeni yeyote yule bila kibali cha mwalimu wa zamu. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi akikamatwa **atafukuzwa shule**.

11. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuwa na kisu, panga au kitu chochote cha hatari Bwenini.

12. Mawasiliano yote yatakuwa katika lugha ya Kiingereza.

13. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na aina ya mavazi yanayoashiria makundi fulani, yenye picha za mapenzi, matangazo ya vikundi vya kigaidi au kapero na simu. Mwanafunzi atakayekamatwa na vitu hivyo, Shule itavitaifisha, naye atachukuliwa hatua kali.

B

DAYOSISI YA KASKAZINI MASHARIKI
KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
SHULE YA SEKONDARI LWANDAI
S.L.P. 01, MLALO,

## KIAPO

A: Mimi ...........................................ambaye nitakuwa mwanafunzi katika shule yako, nimesoma na kuelewa mahitaji na masharti ya shule. Ninakubali kutimiza maagizo na kufuata masharti na sheria zote za shule pia nitasoma kwa bidii ili kutumia nafasi niliyoipata.

...................................
**SAINI YA MWANAFUNZI**

B: Mimi .....................................................ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ...................................................nitahakikisha mtoto wangu ninamlipia fedha za ada na michango kama ilivyooneshwa kwenye barua ya kujiunga bila kukosa. Pia ninaungana na mwanafunzi huyu katika kiapo chake, maana nimesoma na kuelewa kanuni, masharti na sheria za shule.

.................................
**SAINI YA MZAZI/MLEZI.**

C: Barua na taarifa za maendeleo ya mwanangu zitumwe kwa

Jina: .....................................................

Anuani yake: ..............................................

..............................................

Simu ..............................................

N.B. 1. Fomu hii ijazwe na itumwe shuleni kabla ya tarehe 30/06/2021. Au aje nayo siku ya kufungua shule.
2. KUMBUKA PESA YA HUDUMA YOYOTE IKISHALIPWA HAIRUDISHWI ZINGATIA HILO ILI KUEPUKA USUMBUFU.

C

NORTH EASTERN DIOCESE
EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
LWANDAI SECONDARY
S.L.P. 01, MLALO

## MEDICAL FORM

**Ref. No...............................**
**To the medical Officer,**
**...........................**
**...........................**

**REF:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS**

Please examine the above named pupil and give report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

1. Pupils full name .......................................Age .................
2. Blood................................................
3. Stool.................................................
4. T.B Test..............................................
5. Syphilis Test.........................................
6. Urine examination ..................................
7. Eye Test..............................................
8. Chest Test...........................................
9. Ears Test............................................
10. Spleen..............................................
11. Abdomen...........................................
12. Pregnancy (for girls only)......................

ANY ADDITION (INFORMATION: Please defects or impairment, infection, family diseases etc.......................................................................................
...........................................................................................................
...........................................................................................................

I certify that the above pupils are suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons...............................................................................
...........................................................................................................

Name of M.O......................................Signature of M.O.......................
Date ................................................Official stamp..............................

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

A) Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya **Elimu na. 25** ya mwaka **1978**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na waizara yenye dhamana ya Elimu nchini.. Lengo la shule hii pia ni kutoa vijana walioelimika vizuri na wenye TABIA NJEMA INAYOZINGATIA MAADILI MEMA. Wanatakiwa kuonyesha jinsi gani wanaweza kutumia UJUZI na MAARIFA waliyoyapata kwa manufaa ya Taifa na manufaa yao binafsi. Unapaswa kuzingatia yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa kirefu utakapowasili shuleni

## B) BAADHI YA SHERIA ZA SHULE

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria katika shughuli zote za kila siku. Sala ya asubuhi na jioni bila kukosa.
b) Heshima kwa walimu, viongozi, wafanyakazi wasio walimu, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
c) Kila mwanafunzi sharti aepuke na kuchukia vitendo vyovyote vya uongo, uzushi, wizi , uasherati, ulevi, uvutaji sigara na uchoyo.
d) Vipindi vyote vilivyopo kwenye ratiba ya shule ni lazima uvihudhurie bila kukosa pamoja na shughuli za nje ya darasa.
e) Kuzingatia mipaka ya shule na kuhakikisha uko ndani ya mipaka ya shule wakati wote.
f) Kutunza usafi wa mwili, majengo na mazingira kwa ujumla na kuepuka kuzalisha taka na kutupa taka hovyo.
g) Mwanafunzi atatakiwa kulipa Ada na Michango ya shule mara tu afikapo shule. Yeyote atakayebaki na ada (pay in slip ) mfukoni atarudishwa nyumbani mara moja.
h) Kuvaa sare za shule wakati wote, sare isivaliwe na urembo wowote kama vile pete, mikufu, hina, ndevu, kucha ndefu, lipstick n.k.
i) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia vifaa vya umeme kama vile pasi, heater, jiko la umeme, n.k
j) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki wala kutumia simu ya mkononi wakati wote awapo shule.
k) Ni marufuku mwanafunzi yeyote kutembelea mabweni yasiyo ya jinsia yake
l) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea nyumba za walimu au wafanyakazi wa shule bila idhini.
m) Ni marufuku wanafunzi kuwa na silaha ya aina yoyote bwenini.
n) Kila mwanafunzi anatakiwa kufikia wastani wa shule kila ifikapo mwisho wa muhula ambao ni kiwango cha wastani wa **C. (Chini ya hapo atalazimika kukariri darasa).**
o) Mawasiliano ya aina yoyote kati ya mwanafunzi na wenzake au mwalimu ni kwa lugha ya kiingereza tu.
p) Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (*preparation*) ni lazima

## C) MAKOSA YANAYOWEZA KUKUFUKUZA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji, Usagaji na Ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya vikiwemo uvutaji bangi, sigara na kubeli.
4. Kupiga au kupigana
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya **UMMA**
6. Kudharau wimbo na Bendera ya Taifa
7. Kupata mimba au kumpa mimba mwanafunzi au mwanamke yeyote
8. Kuoa mimba au kuolewa
9. Kugoma, kuchochea mgomo, kuongoza na kuvunja amani na usalama wa shule
10. Kukataa adhabu kwa makusudi kutoka kwa viongozi au walimu.
11. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa toka mamlaka husika
12. Utoro wa aina yoyote, kulala nje ya shule bila ruhusa, na
13. Kuonekana katika kumbi za starehe na nyumba za kulala wageni.
14. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.